

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"
Telephone: + 028 2750271
Fax: + 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P 170,
MASWA,
SIMIYU.

Kumb.Na. MDC/ADM/10/30/VOL 1/87

25 Mei, 2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imepata idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kupitia barua Kumb. Na.FA.97/288/01/09 ya tarehe 13/05/2022, iliyotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Maswa anatangaza nafasi za kazi ya **Katibu Mahsusi Daraja la III** kwa Masharti ya kudumu, Hivyo Watanzania wote wenye sifa hizo mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:-

1.0 KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III – NAFASI MBILI (2)

1.1. Sifa za Kitaaluma kwa Mwombaji:-

- Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliohudhuria Mafunzo ya Uhaziri na kufaulu mtihani wa Hatua Tatu. Wawe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na wawe wamepata mafunzo ya komputa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali katika Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-Mail na Publisher na kupata cheti.

1.2. MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka mbalimbali.
- (ii) Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- (iii) Kupokea majalada, kuyagawa na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- (iv) Kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi.
- (v) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Mwajiri au Msimamizi wake wa kazi.

1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara: Ngazi ya TGS B kwa mwezi.

3.0. MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji waambatanishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji ambao wapo kwenye Ajira, barua za maombi zithibitishwe na Waajiri wao.
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

4.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI


Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
S.L.P. 170,
MASWA –SIMIYU.

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 10.06.2022 Saa 9.30 Alasiri.**

NB:

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri www.maswadc.go.tz Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.


MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
Simon Birege
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA**